TANGAZO LA SERIKALI NA.143 la tarehe 3/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA 355)

# AMRI

*(Imetolewa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA PAHI YA MWAKA, 2023.

Jina:

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Pahi ya mwaka, 2023

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura (355)

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji)kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpangokina wa eneo

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Mpango wa Urasimishaji lipo ndani ya Mipaka ifuatavyo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba PH1 yenye majira - nukta 823316MS, 9479169KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini -Mashariki katika uelekeo wa KZ80$^0$46'07''MS kwa umbali wa kilomita 0.850 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba PH2 yenye majira - nukta 824154MS, 9479025KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS11$^0$55'08''kwa umbali wa kilomita 1.287 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba PH3 yenye majira - nukta 824049,MS 9477741KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS75$^0$43'11''MG kwa umbali wa kilomita 0.637 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba PH4 yenye majira - nukta 823438, 9477565; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa KS14$^0$55'05''MG kwa umbali wa kilomita 0.951 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba PH5 yenye majira - nukta 823053MS, 9478434KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ69$^0$24'14''MG kwa umbali wa kilomita 0.548 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba PH6yenye majira - nukta 822565MS, 9478686KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ14$^0$55'05''MG kwa umbali wa kilomita 0.348 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba PH7 yenye majira - nukta 822634, 9479029; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibikatika uelekeo wa KZ80$^0$45'08''MG kwa umbali wa kilomita 0.699 hadi ulipoanzia."

Dodoma
6 Februari, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*